

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Septemba 13, 2022

**MKUU WA WILAYA YA LUDEWA AMEFUNGUA RASMI MAFUNZO YA JESHI LA AKIBA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere akiwakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa Bwn. Linus Malamba leo Septemba 13, 2022 amefungua mafunzo ya Jeshi la Akiba yanayoendelea katika Kata ya Luilo.

Wakati akifungua mafunzo hayo amewapongeza vijana wote waliojiunga na mafunzo hayo zaidi ya vijana 125 wa Kata ya Luilo yenye vijiji vitatu ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Lifua, Luilo na Kijiji cha Kipangala.

Katika hatua nyingine Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ludewa amewasisitiza vijana hao kuwa “ ***nitumie nafasi kuwapongeza wote mliopo hapa, na hakikisheni mnahitimu mafunzo haya kwani fursa za ajira ni nyingi kwasababu zaidi ya makampuni 3 yapo Wilayani kwetu na kwa sehemu kubwa makampuni hayo yanahitaji ulinzi na walinzi wenyewe ndio ninyi mtakaomaliza mafunzo***”.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa.**